

## Nchi Wanachama

Mashirika yanayojumuishwa katika World Bank Group [Mshikano wa Benki ya Dunia] yanamilikiwa na serikali za nchi wanachama, ambazo zina uwezo wa uamuzi katika shughuli zote za mashirika haya-iwe ni shughuli za sera, mambo ya fedha, na hata maswala ya uwanachama.

International Bank for Reconstruction and Development (IBRD) [Benki ya Kimataifa ya Marekebisho na Maendeleo], ina nchi wanachama 184, jumuiiko la karibu nchi zote duniani. International Development Association (IDA) [Shirikisho la Kimataifa la Maendeleo] lina wanachama 163, International Finance Corporation [Muungano wa Kimataifa wa Fedha] lina wanachama 175, Multilateral Investment Guarantee Agency [Shirika la Uthibiti wa Uwekezaji] lina wanachama 158, na International Centre for the Settlement of Investment Disputes [Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Mizozo ya Uwekezaji] kina wanachama 134.

Kulingana na [Articles of Agreement](#) [Vifungu vya Maelewano] vya IBRD, ili nchi iwe mwanachama wa Benki ni wajibu kwanza ijiunge na [International Monetary Fund \(IMF\)](#) [Shirika la Fedha Duniani]. Uwanachama katika IDA, IFC na MIGA ni wajibu kwa kuwa mwanachama wa IBRD. Angalia [Taarifa za Jumla kuhusu Uwanachama](#) kwa habari zaidi za jinsi ya uwanachama na kujisajili katika kila shirika.

Kuna Idara ya Usimamizi katika Benki ya Dunia ambayo husimamia shughuli za wenye hisa. Na katika idara hii pia kuna [Idara ya Uwanachama na Usajili](#) inayoshughulika na uwanachama upya.

Nchi wanachama zinasimamia Mshikano wa Benki ya Dunia kupitia [Board of Governors](#) [Bodi za Magavana] na [Executive Directors](#) [Wakurugenzi Watendaji]. Makundi kaya hupitisha uamuzi wote wa haya mashirika.

### Taarifa za Jumla

[Taarifa za Jumla kuhusu Uwanachama](#)  
[Uwezo wa Kura](#)

### Orodha za Uwanachama

[Orodha ya Uwanachama wa Mshikano wa Benki](#)  
[Orodha ya Uwanachama wa IBRD](#)  
[Orodha ya Uwanachama wa IDA](#)  
[Orodha ya Uwanachama wa IFC](#)  
[Orodha ya Uwanachama wa MIGA](#)  
[Orodha ya Uwanachama wa ICSID](#)